Kijarida Kuhusu

Mihimili ya Dola

Kimeandaliwa na:

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

© LHRC

Septemba, 2013

Yaliyomo

SHUKURANI.....iv

UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU.....v

MAONO.....vi

TAMKO LA LENGO MAHUSUSI.....vi

LENGO KUU.....vi

DIBAJI.....vii

1.0: UTANGULIZI.....1

2.0 MIHIMILI YA DOLA NI IPI?..... 2
2.1 Mahakama ni Nini?..... 2
2.2 Nini Uhuru wa Mahakama?.....2
2.3 Kazi za Mahakama..... 5

3.0 SERIKALI.....5
3.1 Kazi za Serikali.....5

4.0 KAZI ZA BUNGE..... 6

5.0 UTAWALA WA SHERIA..... 6
5.1 Vitu Muhimu vya Kuzingatia katika Utawala wa Sheria..... 8

6.0 MGAWANYO WA MADARAKA..... 9

7.0 BUNGE KUSHIKA HATAMU.....10

8.0 HITIMISHO.....10

SHUKURANI

Tunatoa shukurani kwa wanasheria wetu na wale wa kujitolea katika uandaaji wa vijarida hivi. Pia tunawashukuru kwa dhati wale wote walioshiriki kwenye kukirejea kijitabu hiki ili kuandaa toleo hili la tatu hususan Wakili Harold Sungusia, Wakili Fulgence Massawe, Wakili Jeremiah Mtobesya, Bw. Rodrick Maro na Bw. Evans Sichalwe, pamoja na wafanyakazi wote wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika binafsi la kujitolea na la hiari ambalo si la kisiasa wala kibiashara. Kituo kimeandikishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania mnamo Septemba, 1995. Kabla ya kusajiliwa kama chombo huru, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilikuwa ni mradi wa haki za binadamu wa Mfuko wa Kuendeleza Elimu ya Sheria Tanzania

(TANLET). Makao makuu ya Kituo ni Dar es Salaam na Arusha kuna ofisi ndogo.

MAONO

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina tamani jamii yenye haki na usawa.

TAMKO LA LENGO MAHUSUSI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali wala kibiashara linalojibidisha kukuza uwezo wa jamii ili iweze kukuza, kuendeleza na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini Tanzania.

LENGO KUU

Lengo kuu la Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni kukuza uelewa wa sheria na haki za binadamu kwa jamii kwa ujumla na hasa wale wanajamii ambao kwa sababu moja au nyingine wameachwa nyuma. Uelewa utakuzwa kwa njia ya elimu ya uraia na msaada wa sheria.

DIBAJI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina kazma ya kusaidia jamii ya watanzania kuwa na uwezo wa kufahamu sheria za nchi pamoja na kufahamu haki zao ili kuzilinda na kuzitetea pamoja na kuheshimu haki za wengine ili hatimaye tuwe na jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu pamoja na nchi inayoheshimu utawala wa sheria.

Tunafahamu kuwa kwa raia wa kawaida si rahisi kuzifahamu sheria zetu zote, na hata baadhi tu ya sheria zinazomgusa kutokana na mfumo tulio nao, ambao hautoi nafasi kwa watu wote kujua sheria. Hali hii inasababisha watu wengi kujikuta katika matatizo ya kisheria ambayo yangeweza kuepukika kama angejua sheria. Ndio maana basi Kituo kimeamua kutoa machapisho haya na mengine, kwa lengo la kutoa msaada wa kisheria kwa raia.

Huu ni usaidizi kisheria unaotoa maelezo mafupi na ya msingi ya kisheria ili kukusaidia ndugu msomaji uweze kupata ufumbuzi au maelekezo ya

tatizo linalokusibu. Ni lengo letu kuwa, katika vijitabu hivi tunatoa usaidizi wa moja kwa moja kwako wewe pale utakapokuwa na tatizo au mmoja wa ndugu au jamaa zako wanapopata matatizo ya namna hii.

Tunachokuomba ni wewe kusoma kwa makini; na pale suala lako linapokwenda mbali zaidi ya maelezo haya, basi utafute msaada wa kisheria au uende kwa mwanasheria aliye karibu na wewe ili aweze kukusaidia. Tunaamini utapata usaidizi huu kiurahisi zaidi na maelezo yaliyomo humu yatakusaidia kwa karibu. Umalizapo, tafadhali umsaidie na mwenzako kupata usaidizi huu.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

1.0: UTANGULIZI

Utawala wa nchi huendeshwa na taasisi inayoitwa dola. Taasisi hii huhodhi mamlaka ya aina tatu ambayo ni Serikali, bunge na mahakama. Wajibu wa Serikali ni kuendesha utawala na utekelezaji wa kila siku wa shughuli za umma, bunge linao wajibu wa kujali sera na kutunga sheria na mahakama zinao wajibu wa kusikiliza na kuamua kesi na pia kutoa tafsiri ya sheria na katiba ya nchi.

Mgawanyo huu wa mamlaka ya dola ulifanywa makusudi ili kupunguza uwezekano wa kuzuka utawala wa kidikteta pale itakapokuwa kwamba mtu mmoja au kikundi kimoja cha watu wanahodhi aina zote tatu za mamlaka ya dola kwa wakati mmoja. Ilionekana kuwa ni bora kugawanya aina hizi tatu za madaraka na kuziweka mikononi kwa watu au vikundi vya watu tofauti ili watumiapo mamlaka haya kila mmoja au kila kikundi, kimoja, kudhibiti na kuweka uwiano wa kimizani dhidi ya utendaji wa mtu au kikundi kingine.

Kwa mantiki hii kila mamlaka inaitwa muhimili wa dola na kila muhimili hufanya kazi zake kwa uhuru. Uhuru huu unamaanisha kuwa chombo kimoja kisiingilie kazi za chombo kingine. Ila wakati mwingine kukiwa na kitu kama kutupia macho chombo kingine ili kisitumie vibaya huo uhuru.

2.0 MIHIMILI YA DOLA NI IPI?

Dola yoyote ina mihimili mikuu mitatu nayo ni:-

1. Serikali;
2. Bunge; na
3. Mahakama.

Mihimili hii inaongozwa kwa kanuni kuu moja ambayo ni kutoingiliana katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya kila mhimili. Kila mhimili utafanya kazi zake bila kuingiliwa na mhimili mwingine au kuingilia majukumu ya mhimili mwingine.

2.1 Mahakama ni Nini?

Mahakama ni mhimili wa dola wenye mamlaka ya kusikiliza migogoro yote ya kisheria na kufikia maamuzi juu ya migogoro hiyo. Ni chombo kinachofafanua na kutafsiri sheria.

2.2 Nini Uhuru wa Mahakama?

Uhuru wa Mahakama maana yake ni pale kila jaji au hakimu, anapokuwa huru kuamua mashauri yoyote yanayopelekwa mbele yake kwa kuyatathimini kulingana na ukweli/maelezo ya mashauri hayo na uelewa wake wa sheria bila ushawishi, mvuto au motisha na bila msukumo kutoka kwa mtu au chombo chochote kwa sababu yoyote ile. Hii ni kutokana

na kiapo wanachokula kwa lengo la kutenda haki bila woga au upendeleo na bila tabia ya kujifanya au kujisingizia. Pia katika hilo hawapaswi kufanya maamuzi yao kwa nia ovu (mbaya).

Mahakama kuwa huru haina maana tu kutoingiliwa na bunge na serikali, bali pia iwe huru bila kuingiliwa na mvuto wa kisiasa, dini, jinsia kabila au rangi ya mtu.

Ili kulinda uhuru wa mahakama, lazima mambo yafuatayo yawepo na kutimizwa:-

i. Serikali inawajibika kuweka ndani ya katiba ya nchi vifungu madhubuti vilivyokutwa katika katiba juu ya wakati/muda wa kushika nyadhifa za majaji, usalama, nyadhifa zao, mishahara yao pamoja na uhuru wao;

ii. Pili serikali lazima iachie mahakama masuala yote ya utoaji wa haki za watu. Hata hivyo uhuru wa mahakama siyo leseni ya hakimu au jaji kutimiza masuala ya kisheria kama anavyopenda yeye. Ni lazima afuate matakwa ya sheria na pia taratibu za utoaji wa haki. Zipo kanuni saba za mwongozo wa uhuru wa mahakama kama ifuatavyo:-

    1. Uhuru wa mahakama lazima uhakikiwe na serikali na uhifadhiwe sana katika katiba au sheria za nchi;

2. Mahakama zitaamua mashauri yaliyopo mahakamani kwa uadilifu bila upendeleo wowote;
3. Mahakama zitakuwa na himaya ya mamlaka (jurisdiction) juu ya mambo yote ya haki na zitakuwa na mamlaka za pekee kuamua kama suala lililowasilishwa kwa ajili ya uamuzi wa mahakama liko ndani ya uwezo wake kama ilivyoainishwa na sheria;
4. Hakutakuwa na kuingiliwa kwa mahakama na maamuzi yaliyofikiwa na mahakama, hayatafanyiwa mapitio na chombo au mtu mwingine yeyote;
5. Kila mtu atakuwa na haki ya kushitaki au kushitakiwa katika mahakama za kawaida au kwenye mabaraza yaliyowekwa kisheria kwa mujibu wa taratibu za kisheria;
6. Idara ya mahakama ihakikishe mashauri ya kisheria yanaendeshwa kwa haki bila upendeleo na kwamba haki za wahusika katika mashauri zinaheshimiwa;
7. Ni jukumu la kila nchi mwanachama wa jumuiya ya kimataifa kutoa rasilimali za kutosha kuiwezesha idara ya mahakama kufanya kazi zake vizuri;

Mahakama zitakuwa na mamlaka ya mwisho ya kutamka fasiri ya sheria na pia mamlaka ya kuangalia vyombo vingine vya dola vinafanya kazi zao ipasavyo.

2.3 Kazi za Mahakama

a) Kutoa tafsiri ya sheria;

b) Kuangalia vyombo vingine vya dola kama vinafanya kazi zao ipasavyo.

3.0 SERIKALI

Serikali ni mojawapo ya mihimili mitatu ya dola. Kwa kawaida serikali ndiyo mtendaji mkuu wa kuiwezesha mihimili mingine ifanye kazi. Kwa mfano, serikali ndiyo inayotoa fedha ili kuiwezesha mihimili mingine kutekeleza majukumu yake.

3.1 Kazi za Serikali

a) Kusimamia utekelezaji wa sheria;

b) Kulinda raia wake kwa kuweka ulinzi thabiti uwezeshao raia wake kuwa huru muda wote;

c) Kusimamia amani;

d) Kuiwezesha nchi kuwa na mapato ya kutosha kujiendesha katika shughuli mbalimbali mfano ukusanyaji wa kodi;

e) Kuwezesha raia wake kupata ajira.

Kuangalia vyombo vingine vya dola kama vinafanya kazi zake ipasavyo.

4.0 KAZI ZA BUNGE

a) Kutunga sheria;

b) Kuwasilisha wananchi wa majimbo yao bungeni, kwa kuihoji na kuiuliza serikali masuala yanayogusa maslahi ya wananchi;

c) Kupitisha bajeti ya serikali baada ya kuijadili na kuridhika nayo;

d) Kuiwajibisha serikali katika utendaji wake wa kazi; na

e) Kujadili na kupitisha sera za umma.

5.0 UTAWALA WA SHERIA

Utawala wa sheria ni msingi mkuu wa utawala bora, msingi huu unapaswa kuzingatiwa na mihimili yote mitatu ya dola (Mahakama, Bunge na Serikali). Maana halisi ya utawala wa sheria na taasisi zake zote ikiwa ni pamoja na wateja wake wote kuheshimu katiba ya nchi na sheria zake na kuzilinda. Dola na taasisi zake vinapotii sheria na katiba ya nchi katika kuendesha shughuli za kila siku ndio raia wanapowajibika kwa upande wao kujua katiba na sheria za nchi, kuzitii na kuzifuata katika shughuli zao za kila siku.

Utawala wa sheria unahitaji watu wote kutendewa sawa mbele ya sheria. Usawa mbele ya sheria ina maana kuwa kila mtu atendewe sawa na mwingine na taasisi za dola bila kubagua kwa misingi ya rangi, dini, kabila, jinsia, au tabaka. Sheria isitungwe kufaidisha tabaka fulani la jamii au kukandamiza tabaka jingine.

Vipengele vikuu vya utawala wa sheria ni kama ifuatavyo;-

i. Kazi zote za serikali ambazo zinaweza kuathiri haki za msingi za watu zitekelezwe kwa kuzingatia masharti ya haki za binadamu yaliyoainishwa ndani ya katiba ya nchi, sheria na mikataba mbalimbali ya kimataifa ya haki za binadamu;

ii. Utawala wa sheria unaitaka serikali na idara zake nyingine kwamba sheria isitoe upendeleo usio wa lazima kwa serikali na vyombo vyake. Kanuni hii ni lazima ifuatwe kwa sababu serikali ikipata upendeleo kama huo itaacha wajibu wake wa kufanya kazi kwa kufuata sheria. Kwa kufanya hivyo haki za watu zitakuwa hatarini;

iii. Utawala wa sheria pia una maana kuwa hakuna mtu atakayeadhibiwa kwa kosa la jinai kama hakuna sheria iliyoainisha kosa hilo, na wala

sheria haitatoa adhabu isiyowiana na kosa lililotendwa;

iv. Lazima pawepo na mipaka ya utumiaji wa nguvu za serikali katika utendaji wake wa kila siku. Matumizi ya nguvu ya utashi (*discretion*) lazima yafanywe kwa misingi ya kisheria;

v. Sheria zenye kutoa adhabu, kuondoa au kupunguza nafuu kwa raia zisitungwe na kutumika kwa kipindi kilichokwishapita. (kinyumenyume);

vi. Maamuzi yote yanayogusa haki za mtu binafsi yafanywe kwa kuzingatia haki za asili.

ANGALIZO

Utawala wa sheria si tu kwa serikali kufuata sheria na kuheshimu uhuru wa mahakama, bali pia kuheshimu haki za watu binafsi na uhuru wao. Huo ndio msingi mkuu wa utawala wa sheria. Ni lazima pia haki za wananchi katika maendeleo zizingatiwe barabara.

5.1 Vitu Muhimu vya Kuzingatia katika Utawala wa Sheria

1. Kwamba hakuna mtu atakayeadhibiwa au katika kuingizwa hasara isipokuwa tu atafanyiwa mambo hayo kama atavunja sheria inayoeleweka

iliyotungwa katika taratibu za kawaida za kisheria na ataadhibiwa mbele ya mahakama za kawaida za nchi;

2. Kwamba hakuna taasisi ya dola au binafsi au mtu aliye juu ya sheria;
3. Kwamba haki ya uhuru wa mtu binafsi ni ya msingi katika utawala wa sheria.

6.0 MGAWANYO WA MADARAKA

Mwanzo wa kitini hiki imeelezwa kwamba mamlaka ya dola ya kutawala imegawanywa katika mihimili mitatu ambayo ni serikali, bunge na mahakama.

Kwa mfano, ni hatari mtu au chombo kimoja kutunga sheria, kisha kupewa mamlaka ya kuitekeleza sheria na kisha kuamua migogoro inayotokana na malalamiko ya wananchi dhidi ya sheria hiyo. Kwa mfano huu, itakuwa sawa kama kumpa mkosaji mamlaka ya kujihukumu mwenyewe au kupeleka kesi ya ngedere ikaamuliwe na nyani.

Tafsiri hiyo hapo juu ina maana kuwa watu wenye mamlaka ya aina moja wasishiriki kwenye utendaji wa muhimili mwingine kati ya mihimili mitatu ya dola. Yaani kila muhimili usiendeshe au kuingilia kazi za muhimili mwingine. Jambo la muhimu hapo ni kila muhimili kuangalia mwingine unafanya vipi kazi kwa mujibu wa sheria.

7.0 BUNGE KUSHIKA HATAMU

Kwa ujumla bunge lina haki ya kutunga au kufuta sheria yoyote. Hakuna mtu au chombo chenye mamlaka ya kutunga sheria isipokuwa kwa mtu au chombo hicho kinaruhusiwa kutunga sheria hiyo na bunge. Kwa hiyo katika hali ya kawaida bunge ndio chombo chenye mamlaka ya juu kabisa ya utungaji wa sheria. Bunge laweza kutunga, kubadilisha, kurekebisha au kufuta sheria yoyote ile ya nchi.

Hata hivyo ieleweke wazi kwamba bunge linapaswa kutunga sheria ambazo hazipingani na matakwa ya Katiba ya nchi. Ikiwa bunge litatunga sheria inayovunja vipengele vya katiba, mahakama zina uwezo wa kutamka kwamba sheria hiyo ni kinyume cha katiba na hivyo kuibatilisha na kuitupilia mbali.

8.0 HITIMISHO

Ingawa kuna mgawanyo wa madaraka katika mihimili ya dola, ukiangalia kwa undani zaidi utagundua kuwa kuna kuingiliana kwa namna moja. Kwa mfano mahakama inaweza kutoa matamko kwamba sheria fulani ni batili na hivyo kutupilia mbali pale inapoonekana imekiuka misingi fulani ya katiba. Katika hali ya kawaida bunge ndicho chombo cha kubadili au kufuta sheria na siyo mahakama. Vilevile

mahakama zaweza kuingiliwa na serikali katika utendaji wake, kwa mfano maofisa wa juu kabisa wa mahakama yaani majaji na wasajili wa mahakama ambao huteuliwa na Rais wa nchi, hivyo ingawa wamekingwa kikatiba kutokuondolewa nyadhifa zao ovyo ovyo. Bado pia kuna udhaifu wa kibinadamu wa kuamua kesi kwa kupendelea serikali ili mahakimu au majaji wapandishwe vyeo. Pia utaona kuwa serikali ndiyo inayopeleka miswada bungeni ambayo mara nyingi hupitishwa na bunge kama ilivyopelekwa au kufanyiwa marekebisho kidogo sana. Hivyo bunge linakuwa ni kama mhuri tu wa kupitisha maamuzi ya serikali kuwa sheria. Pia watumishi mbalimbali wa serikali hupewa mamlaka ya kutunga sheria, kazi ambayo inapaswa kufanywa na bunge.

Hata hivyo, pamoja na muingiliano huo, bado tunaweza kusema ni jambo lisiloepukika kwani kama isipokuwa hivyo basi itakuwa ni kama kuna serikali tatu ndani ya dola moja. Ni dhahiri kuwa kila mhimili ndani ya dola utakuwa macho kuangalia na hata kukemea jambo fulani linalofanywa na mhimili mwingine. Ndio maana mahakama ina mamlaka ya kutamka sheria fulani ni mbaya kwa sababu inakiuka msingi ya haki za binadamu au iko kinyume cha katiba. Kwa kufanya hivyo inakuwa imeangalia na kudhibiti kazi za bunge. Bunge linapaswa

kurekebisha sheria hiyo ili ikidhi mahitaji ya katiba. Bunge nalo linaangalia bajeti ya serikali na kufanyia marekebisho pale inapostahili, kwa hiyo ni wazi kwamba mfumo una kila chombo kuangalia kingine ambao ni wa muhimu katika uendeshaji wa shughuli za kila siku za dola.

Ni matumaini yetu kuwa ndugu msomaji mpaka sasa unaufahamu wa kutosha kuhusu mihimili mitatu ya serikali ambayo ni mahakama, bunge na serikali inavyofanya kazi. Ombi letu ni kwamba tunaomba unapomaliza kusoma kijarida hiki utoe elimu uliyopata kwa watu wengine ili nao pia wapate kufahamu mihimili ya dola na kila mmoja unavyofanya kazi.